



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

CHUO CHA UHASIBU ARUSHA



TAARIFA KWA UMMA

Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kinapenda kuutarifu Umma kuwa kuanzia tarehe 3, Agosti 2018 malipo yote kwa ajili ya huduma mbalimbali zitolewazo na Chuo yatafanyika kwa njia ya Kielektroniki kupitia mfumo ulioanzishwa na serikali ujulikanao kama Government e-Payment Gateway (GePG).

Kwa sababu hiyo, Wanafunzi pamoja na wadau mbalimbali wanatakiwa kutumia nambari ya kumbukumbu ya malipo (Control Number) **994100000009** kwa ajili ya kufanya malipo yoyote.

Namna ya Kulipa kwa Kutumia mfumo wa Kielektroniki (Government e-Payment Gateway):

- 1) Tumia nambari ya kumbukumbu ya malipo (Control Number) **994100000009** kufanya malipo. Nakili namba hii ya uhibitaji na tembelea Tawi lolote la Benki ya CRDB, NMB, au NBC ili kulipa. Baada ya kuwasili kwenye benki, mpe mtoa huduma wa dirishani namba ya kumbukumbu ili kukamilisha mchakato wa malipo yako.
- 2) Malipo yanaweza pia kufanywa kwa njia ya mtandao wa simu za mkononi (M-Pesa, Tigo-Pesa, na Airtel Money) kwa kufuata hatua zifuatazo:
 - a. Kutoka kwenye simu yako, piga simu *150*00#, au *150*01#, au *150*60# (Ili kupata Menu ya M-pesa, Tigo-Pesa, na Airtel Money kwa mtiririko huo);
 - b. Chagua "Lipia Malipo (Pay Bills)";
 - c. Chagua "Malipo ya Serikali";
 - d. Chagua "Ingiza namba ya malipo" na uingize namba ya malipo **994100000009**;

- e. Weka kiasi cha fedha unachotaka kulipa;
- f. Thibitisha muamala wako kwa kuingiza neno au namba yako ya siri;
- g. Hifadhi ujumbe wa simu uliopokea kama ushahidi wa malipo endapo utahitajika kuonyesha kwa taasisi.

**MKUU WA CHUO,
CHUO CHA UHASIBU ARUSHA,
S. L. P. 2798,
ARUSHA.**

TEL: 255 027 2501415/6, 2549264, 2546096/254 9605-6; 0784-542778

www.iaa.ac.tz | iaa@iaa.ac.tz